**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA**

TPHPA

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

# TAARIFA KWA UMMA

## KUONDOLEWA KWA VIUATILIFU HATARISHI KATIKA SOKO LA TANZANIA

**07 Januari, 2026 Arusha**

Viuatilifu ni miongoni mwa pembejeo muhimu katika uzalishaji wa mazao ya kilimo nchini Tanzania ambavyo hutumika kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao, magugu na magonjwa ya mimea hivyo kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo. Kuongezeka kwa tija kunachangia upatikanaji endelevu wa chakula, lishe bora, malighafi ya mazao ya kilimo na mapato ya fedha za kigeni. Hata hivyo, pamoja na umuhimu wake, Viuatilifu visipotumika kwa usahihi na kwa usalama vinaweza kusababisha madhara kwa afya ya binadamu, wanyama na mazingira.

Ili kudhibiti athari zinazohusiana na matumizi ya Viuatilifu, Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), kupitia Sheria ya Afya ya Mimea (Sura ya 133) na Kanuni zake za mwaka 2023 (pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2024), imepewa jukumu la kusimamia uingizaji, usambazaji, na matumizi ya Viuatilifu nchini.

Pamoja na Sheria ya Afya ya Mimea, Tanzania pia ni mwanachama wa mikataba ya kimataifa ya usimamizi wa matumizi ya Viuatilifu kama vile *Stockholm Convention, Rotterdam Convention, Montreal Protocol na International Plant Protection Convection (IPPC)* katika kudhibiti athari zinazoweza kusababishwa na Viuatilifu.

Hivi karibuni, TPHPA ilifanya mapitio ya kina ya Viuatilifu vilivyosajiliwa nchini kuainisha Viuatilifu Hatarishi (Highly Hazardous Pesticides; HHPs). Kufuatia mapitio hayo, Mamlaka inaufahamisha Umma kuwa:-

1. Inaondoa sokoni Viuatilifu 130 (Pesticide products) vilivyoainishwa kuwa na viambata hatarishi (HHPs) kwa mujibu wa vigezo nane (8) vya FAO/WHO **(Rejea Jedwali la 1).**
2. Inaondoa sokoni Viuatilifu vyote vyenye Paraquat, Paraquat dichloride, Dimethoate na Acephate **(Rejea Jedwali la 2).**
3. Inaondoa sokoni Viuatilifu 675 ambavyo usajili wake haukuhuishwa kwa kipindi cha miaka kumi na zaidi **(Rejea Jedwali la 3).** Kutokuhuishwa kwa usajili kwa kipindi chote hicho kunadhihirisha Mmiliki kutokuwa na uhitaji wa Kiuatilifu husika.

**Orodha ya viuatilifu vyote vilivyo ondolewa sokoni vikiwemo viuatilifu hatarishi inapatikana katika tovuti ya Mamlaka** www.tphpa.go.tz

Kufuatia kuondolewa kwa Viuatilifu vyenye viambata hatarishi vilivyotajwa katika kipengele cha 1 hapo juu, pamoja na Paraquat, Paraquat dichloride, Dimethoate na Acephate vilivyotajwa katika kipengele cha 2 hapo juu, Mamlaka inapenda kuutarifu Umma kuwa kuanzia tarehe ya taarifa hii:-

1) Hakutakuwa na ruhusa ya kuingiza nchini bidhaa za Viuatilifu vyenye viambata tendaji vilivyotajwa.

2) Usajili wa Viuatilifu vyenye viambata amilifu vilivyotajwa katika vipengele vya 1 na 2 hapo juu hautakubaliwa.

Wafanyabiashara wote walio na akiba ya bidhaa hizo nchini wanaarifiwa kumaliza akiba hiyo ndani ya kipindi kisichozidi miaka miwili.

Hitimisho, Mamlaka inaendelea kutekeleza jukumu lake la kisheria ili kuhakikisha kuwa Viuatilifu vyote vinavyoidhinishwa kutumika nchini Tanzania ni salama kwa Binadamu, Wanyama na Mazingira.

Imetolewa na,

Prof. Joseph C. Ndunguru
**MKURUGENZI MKUU**

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY
P.O. Box 3024, Tel.: +255 27 297 0487
ARUSHA - TANZANIA